

KIKAO

Phone ringing.....

Don't worry kila kitu kinaenda kuisha leo mamii.

Wait, amepokea acha niongee nae.....

Hello brother its Alpha speaking, najua unaweza ukawa unanifahamu kwa namna moja ama nyingine.....

Go direct to the point (ilisikika sauti ya ukali kutoka upande wa pili wa simu)

Cool down brother, wala kulikuwa na haja ya wewe kuniambia hilo kwa ukali maana ndipo nilipokuwa nikielekea.

Ok ni kwamba nahitaji tufanye kikao cha mtu tatu yaani wewe, mimi na mkeo nyumbani kwako asubuhi ya leo.

Sasa hivi ni saa 9:05 asubuhi I will be here waiting for you mpaka saa 10:00 otherwise.....

Nilikata simu

I switched off both my phone and that of Sonia.

Sonia speaking "Alpha what are you planning to do, please usifanye kitu kibaya please."

Sonia hutakiwi kuhofia, today we are going to end this game.....

Upande wa pili

Jamaa aliingiwa na wasiwasi simu ilipokatwa huku
ikimuacha njiapanda.

Akahaha asijue anaanzia wapi huku akiwa na pupa ya
kuwahi nyumbani akajue ni nini anaitiwa.....

Aliwasha gari mkuku mkuku na mnamo saa 9:35 akawa
ameshawasili nyumbani.....

Jamaa aliingia sebuleni mbiombio huku akitukuta mimi
na mkewe tukiwa tunamsubiri sebuleni.....

I smiled na nikamwambia cooldown bro, take a seat...

Omega

I call you by your name....

Najivunia kulala na mkeo,nimevumilia sana na leo
nimeamua kusema sijali kama utanikaba koromeo,
utanivunja na kuniacha kimeo.

Kamwe sijutii katu, sijutii katu piga kelele jaza
umati sihofii watu.....

Nimekubuhu mpaka inafika hatua nimefanya mtaa mzima
unajua

Na sifikirii ni rough, kwa mitindo zaidi ya saba na
maumbile nimejaaliwa sii haba.

Nilimpa raha kote kwenye gari na varanda kama mfungwa
aliyekutana na kahaba.

Ona mume ndago bila kiwewe,kila uliposafiri

Mi nilipiga misele, aliponiita niliitika kuzizima
kelele na nilipofika nilihakikisha anafika kilele.

Alinipeleka mbali kwa misemo motomoto, hadithi njoo
utamu kolea.

Ukihisi naonngeza chumvi kwa maneno ya uongo, ona
alama ya meno kwenye mgongo.

Halafu ngojea ni hakika alinikumbuka kila mida na
aliponihitaji niliibuka bila shida.

Alipopata swali aliniona mimi kwanza akajiita
Juliette nikajiita Romeo, believe that.

Alifika alikaza na kamba, aliweka mizizi ya kukata na
panga.

Alichizika utasema mwehu, moyoni aliacha alama kama
Ronaldo alivyoacha alama Bernabeu

Nilikuwa siufahamu ugoni, aah kama kufumaniwa ni
dhambi na nitapata adhabu motoni, nitaenda na
tabasamu usoni.

Labda wakati ni sasa, nimerudi kuenzi nafasi napenda
uhakika sipendi bahati naomba ujue kuwa mkeo
hakupendi kwa dhati, kumlazimisha ni kumuenzi hayati.

Sasa kwa nini usinipige na ulivyojifugua
misuli, nivunje mbavu zangu labda utajisikia vizuri.

Fanya maamuzi sasa maana najitia kiburi, niue leo
walimwengu watafukia kaburi.

Najisikia uchovu na mihayo napiga uliza hizi nyayo na
nyika nimetoka mbali fanya maamuzi tuhitimishe kikao
maana hata na mimi nina mishe kibao.

Mishe hata wewe unazo,mishe unazo badili fafanua
eleza na uweke mifano isawili.

Huo ubishi wa kujikweza weka kando ukatili,leo ndio
mwisho nina vunja ndoa yako batili.

Andika talaka ili tuondoke.

Maana maamuzi ni yako au chukua panga unichome.

Haukuitendea haki kura yako, kuchagua ndoa wakati sio
jambo kubwa kwako.

Utakapochukua wasaa utangundua ulimpa saa alipohitaji
muda wako.

Anajua kuwa mkoa wa mbali una watoto,
Anajua kuhusu vikao na safari za uongo, anajua kuhusu
condom ulizobana kwenye nguo na message za wasichana
wa chuo.

Shiiiiit.....

Ulimkuta mwema ukamteka kiakili ukamshawishi mpaka
akakupa shehena ya mwili,

Akakupa moyo akihisi utaweka nadhiri ukajisahau na
ukamuonesha asili ya kwamba wewe ni mchafu kipi
unaropoka lakini,

Ubaya hulipwa kwa ubaya unachokonda ni nini, mmoja
ametupa mwingine ameokota yamkini,

Aliyetupa ni wewe na aliyeokota ni mimi.
ulikuwa ni sababu ya msongo wa Mawazo ndo maana
ukaona wife si wamoto kama mwanzo

Aliteseka kiasi aliona ndoa ni sumu na nikachukua
maamuzi magumu dongo kwako.

Nilimuokoa nikamvusha Bahari, maana muungwana vitendo
maneno hayata angusha Jabari siku mwili hautagusa
sayari.

Utamkumbuka nap engine utajifunza kujali.

Mpunga umeyumba umeanza kujishuku mzee, unarudi
nyumbani baada ya kushindwa kumudu starehe
Haukuwepo kwenye shida ilipofuzu tarehe ulikimbia na
nilikuwepo mimi pekee

Ngoja nikuudhi unajua mwanao ananiita dady nampeleka
shule na namrudisha nyumbani baada ya kazi
Nalipa ada usizokumbuka kutoa, mwanao amefikia
baleghe na nimemfunza kunyoa.

Nimemfunza ushairi nimemfunza kufanya mahesabu,
nimemfunza kufunga tai kisha Kamba za viatu
Nimemfunza sheria zile zinazoongelewa bungeni na
nilienda kumtetea alipoonewa shuleni

Una hoja yoyote defensively, maana hujui kama
wanalala au wanaamka safely

Hujui kuhusu family dinner women's day birthday zao
hujui hata anniversary

Hujui maumivu aliyoyapata moyoni,
Haujui harufu ya chakula alichopasha jikoni

Haujui kuhusu depression maana mara mbili nimemkuta
amejifunga Kamba shingoni

Nampenda yeye amenifanya nipate ishara, amenipa
counselling amenifanya niache sigara

Anajua chakula nikipendacho, timu niipendayo,
kinywaji, anajua even my favorite color

wenzio tunatafuta familia ili tujenge wewe yako ni
lini?

Mkeo amesaliti ndoa sababu yake ni upweke sababu
yako ni nini?

You know when they say what goes around comes around
and that's very true.

So, I wonder why you changed, you used to be a good
man na hapa ni you.

Nakiri mbele za watu nilishiriki hii dhambi
Uvungu wa moyo wangu unasema usaliti ni haki.

Nyanyua kisu chako uniue ila naomba unielewe
sijaivunja ndoa yako umeivunja ndoa yako mwenyewe.....

Na ukitoka hapa utaenda jamiiforums kuwaponda
wanawake na kusema ndoa ni utapeli.....

Nimemaliza kikao, tuondoke zetu Sonia.....